BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 03 Oktoba, 2018.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Ripoti ya Pili ya Utekelezaji wa kazi za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa mwaka 2017/2018.

Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar na kuweka masharti bora yanayohusiana na Kazi, Uwezo, Uongozi na Mambo Mengine YanayohusiAna na Hayo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa mwaka 2017/2018

Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar na kuweka masharti bora yanayohusiana na Kazi, Uwezo, Uongozi na Mambo Mengine YanayohusiAna na Hayo .

III. MASWALI:

Wizara ya Fedha na Mipango:

73. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Mnamo tarehe 9/7/2018, vyombo vya habari vya Serikali (ZBC) vimeripoti kuhusu ujumbe mzito wa Serikali uliokwenda China kushuhudia uwekwaji mkuku wa meli ya mafuta ya SMZ inayojengwa nchini humo.

(a) Je, katika ujumbe huo kumezingatiwa vipi mahitaji ya wataalamu wetu ili yasije kujitokeza matatizo kama ilivyokuwa kwa meli ya M.V Mapinduzi.

(b) Katika ujenzi wa meli hii mpya ya mafuta, Je, ni nani anaeishauri Serikali kuhusu ubora wa ujenzi wa meli hiyo.

126. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Kwa kuwa lengo la Serikali kufikia mwaka wa 2020 iwe tumeifikisha Zanzibar katika uchumi wa kati. Na kwa kuwa moja kati ya vianzio vyetu vya mapato ni kukusanya kodi.

(a) Je, hadi kufikia mwezi Agosti, 2018 ZRB imewasajili wafanyabiashara wangapi kwa Unguja na Pemba ambao wamefikia kiwango cha LTO na wangapi MST.

(b) Je, kuna utaratibu gani unaotumika kupitia mfumo ambao unatumiwa na ZRB wa V.TAX kuweza

kuwabaini wafanyabiashara wanaokwepa kulipa kodi au wanaolipa pungufu.

(c) Je, kuna mashirikiano gani kati ya ZRB na Manispaa, na wafanyabiashara wadogo wadogo na wa kati ambao wanakata leseni za biashara ili wasajiliwe na waweze kulipia kodi kwa mujibu wa sheria.

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto:

69. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto:

Mnamo tarehe 29/06/2018, vyombo vya habari vimeripoti ombi la wazee wa Limbani Pemba kwa Mkuu wa Wilaya ya Wete Bwana Abeid Juma kuwapatia daktari ambaye atawapitia angalau mara mbili kwa wiki.

(a) Je, Serikali imelipokeaje ombi hili.

(b) Je, hatua gani zimechukuliwa na Wizara katika kuratibu ombi hili ili kuwasaidia wazee wa Limbani Pemba wapate daktari huyo.

(c) Je, Wizara imefuatilia ombi hili ili kujua ni lini wazee wa Limbani watapatiwa daktari huyo ili kuwapatia huduma za afya kwa ukaribu.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

120. MHESHIMIWA SULEIMAN SARHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kumejitokeza malalamiko kwamba kuna baadhi ya walimu sio waadilifu ambao hutumia uwalimu wao katika kuwadhalilisha watoto wa kike na wanapokataa huwafelisha masomo yao.

(a) Je, suala hili katika Wizara hii lishawahi kuletwa.

(b) Je, kama bado, mmelifuatilia vyuoni na baadhi ya skuli na kusikiliza malalamiko yao.

(c) Je, kama lipo mnachukua juhudi za aina gani kuliondoa tatizo hilo.

Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

8. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje): - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Eneo la Mji Mkongwe ni urithi wa kimataifa ambapo haiba kubwa ya mji ule ni majengo, watu na tamaduni zinazoambatana na maisha yao. Miaka ya hivi karibuni hali hiyo inaonekana kutoweka kwa kasi kwa eneo la Mji Mkongwe kujengwa hoteli zinazokaribia kuzidi makaazi ya watu na kupoteza ule utamaduni wa asili wa eneo hilo.

(a) Je, ile ahadi ya Serikali kudhibiti ujenzi wa hoteli na migahawa Mji Mkongwe ili kulinda urithi huo wa kale imepotelea wapi.

(b) Kwanini vibali vya ujenzi wa mahoteli vinatolewa na huku Mji Mkongwe unapoteza haiba ya utamaduni wake wa majengo, watu na makaazi.

(c) Je, Serikali haioni utitiri wa hoteli hizo ni hatari kwa Mji Mkongwe kupoteza makaazi ya watu na kugeuzwa kuwa mji wa starehe huku kukiwa na nyumba za ibada, skuli na urithi wa kimataifa.

152. MHESHIMIWA ALI SULEIMAN ALI (Jimbo la Kijitoupele) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati ilifanya zoezi la upimaji wa ardhi na kuleta matumaini juu ya kuondoa migogoro ya ardhi nchini, lakini kwa bahati mbaya zoezi hilo limesimama hadi sasa.

Kwa kuwa zoezi hili ni zuri na linaondoa migogoro ya ardhi nchini, Je, zoezi hilo litaanza lini tena.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

131. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Kwa kuwa msimu wa kilimo cha mpunga 2018, kulikuwa na upungufu wa matreka hasa kwa upande wa Pemba. Na kwa kuwa zipo mashine ndogo ndogo za bei nafuu za "Rice Planting" ambazo bei yake ni kati ya Dola 300 hadi 500 ambapo wakulima wetu wanaweza kukopeshwa, jambo litaloongeza mavuno.

(a) Je, Serikali ina mpango wa kuagiza mashine hizo za kulimia za bei nafuu na kuwakopesha vikundi vya wakulima ili kuongeza uhakika wa chakula.

(b) Je, Wizara imejipanga vipi kwa msimu wa kilimo cha mpunga utakaoanza mapema 2019 ili kuhakikisha wakulima wanapatiwa matrekta na pembejeo nyengine ili waweze kulima mapema na kupata mazao mazuri.

Wizara ya Afya:

18. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB ((Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Hatua kubwa ya maendeleo imefikiwa baada ya kuanzishwa kwa Kitengo cha Matibabu ya figo katika Hospitali ya Mnazimmoja na Serikali inastahili pongezi kwa hatua hii. Hata hivyo wafanyakazi wa kitengo kile wanahitaji kupatiwa mafunzo na vifaa vya kufanyia kazi kama vile “dialers”, “*hypertitis injection”* na “*isopotein”.*

(a) Je, Wizara imeandaa mpango gani wa mafunzo kwa ajili ya wafanyakazi wa kitengo cha matibabu ya figo.

(b) Je, Wizara imejipanga vipi kuhakikisha kuna vifaa muhimu na vya kutosha katika kitengo cha matibabu ya figo.

IV. TAARIFA ZA SERIKALI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Ripoti ya Pili ya Utekelezaji wa kazi za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa mwaka 2017/2018.

V. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar na kuweka masharti bora yanayohusiana na Kazi, Uwezo, Uongozi na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Zanzibar,
03 Oktoba, 2018.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.